TANGAZO LA SERIKALI NA. 564 la tarehe 12/7/2024

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA YA 272)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29 (d))*

AMRI YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA SHINYANGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga ya Mwaka 2024.

Bei na ada

2. Bei na ada za huduma za maji na usafi wa mazingira za Shinyanga zinarekebishwa kwa ajili ya kutumika katika eneo la huduma ikijumuisha Tinde, Didia na Iselamaganzi kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

Masharti

3. Bei na ada zilizoidhinishwa zitazingatia masharti yafuatayo:

(a) Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga ifikapo au kabla ya tarehe 30 Oktoba 2024, itawasilisha kwa EWURA -

(i) mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii; na

(ii) ushahidi kuwa kabla ya kuanza kutumika kwa bei na ada chini ya Amri hii, imetoa taarifa kwa wateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na elimu kwa wadau ikijumuisha viongozi wa serikali, viongozi wa vyama vya siasa na wawakilishi wa taasisi za kidini

na umma kwa ujumla kuhusu marekebisho ya bei za huduma yaliyoidhinishwa;

(b) Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga
   (i) itatekeleza matakwa ya tozo za udhibiti kwa kuwasilisha tozo zilizokusanywa kwa wakati;
   (ii) itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA; na

(c) taarifa zinazorejewa katika aya ya (b) (ii) zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga ikilinganishwa na mamlaka nyingine za maji na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake.

Kufutwa kwa TS Na. 2 la 2019

4. Amri ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (Shinyanga WSSA) ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 inafutwa.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BEI NA ADA ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Matumizi ($m^3$) | Bei za Sasa | Bei zilizoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| | | 2023/24 | 2024/2025 |
| Majumbani | 0-5 | 1,490 | 1,490 |
| | Zaidi ya 5 | 1,740 | 1740 |
| Taasisi | | 2,760 | 2,760 |
| Biashara | | 2,790 | 2,790 |
| Viwanda | | 2,850 | 2,850 |
| Magati | | 1,500 | 1,500 |
| Viwanda vya Maji ya Chupa | | 3750 | 3750 |
| WASTANI | | 2,014 | 2,014 |

Jedwali Namba 1(b):
Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa maunganisho mapya ya maji
(Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya sasa | Ada Iliyoidhinishwa |
|---|---|---|
| | 2023/24 | 2024/2025 |
| Wateja wote | Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama Ilivyoelekezwa kwenye kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | 26,000 |

Jedwali Namba 1(c):
Ada za Sasa na zilizoidhinishwa za kurejeshewa huduma ya maji (Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa |
|---|---|---|
| | 2023/24 | 2024/2025 |
| Majumbani | 10,000 | 10,000 |
| Taasisi | 20,000 | 20,000 |
| Biashara | 20,000 | 20,000 |
| Viwanda | 20,000 | 20,000 |
| Viwanda vya Maji ya Chupa | 50,000 | 50,000 |

Dodoma,
4 Julai, 2024

JAMES A. MWAINYEKULE,
*Mkurugenzi Mkuu*